

# HALMASHAURI YA MJI MAFINGA



29/01/2018

## TANGAZO LA KAZI YA UJENZI WA MAJENGO KATIKA SHULE YA MSINGI MAKALALA

1. MKUU WA SHULE YA MSINGI MAKALALA ILIYOPO HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA ANAWATANGAZIA MAFUNDI WENYE SIFA KWA AJILI YA KUOMBA KUFANYA KAZI ZA UJENZI WA MAJENGO YAFUATAYO KATIKA SHULE YA MSINGI MAKALALA:-

- ) JENGO LA BWENI
- ) JENGO LA BWALO LA CHAKULA
- ) MATUNDU MATANO YA VYOO

2. MUOMBAJI ANATAKIWA AWE NA SIFA ZIFUATAZO:-

- AWE NI MKAZI WA MJI WA MAFINGA.
- AWE NA UJUZI WA KUTOSHA KUFANYA KAZI HIZO ZILIZOTAJWA
- AWE MWAMINIFU NA SI WA KUSIMAMIWA KWA KARIBU SANA
- AWE NA UZOEFU WA KAZI ZA UJENZI NA ZENYE UBORA WA VIWANGO VYA SERIKALI
- AWE NA AKAUNTI BENKI YA NMB AU TAWI LOLOTE HAPA MAFINGA
- AAINISHE KAZI KUBWA MBILI ALIZOFANYA HIVI KARIBUNI NA UJENZI UWE UMEFIKIA ANGALAU ASILIMIA TISINI (90%)

3. RAMANI YA JENGO PAMOJA NA NUKUU ZA BEI (QUOTATION) ZINAPATIKANA OFISI YA MKUU WA SHULE ILIYOPO SHULE YA MSINGI MAKALALA KUANZIA SAA.2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 9: 30 ALASIRI SIKU ZA KAZI.

4. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI **TAREHE 05/02/2018 SAA 6:00 MCHANA**, MAOMBI YOTE YAWASILISHWE OFISI YA MKUU WA SHULE MAKALALA S.L.P 58 MAFINGA, ATAKAYEWASILISHA BAADA YA HAPO MAOMBI YAKE HAYATAFANYIWA KAZI.

5. BARUA YA MAOMBI YA KAZI HIYO IFUNGWE KWENYE BAHASHA VIZURI NA KUANDIKWA ‘OMBI LA KUFANYA KAZI YA KUJENGA JENGO LA (AINISHA JENGO UNALOOMBA) SHULE YA MSINGI MAKALALA’, NA ISIWE NA ALAMA YOYOTE YA KUMTAMBULISHA MUOMBAJI JUU YA BAHASHA.

6. MUOMBAJI ANATAKIWA KULIPIA ADA YA MAOMBI KIASI CHA SHILINGI **30,000.00 (ELFU THELATHINI TU)** KATIKA OFISI YA MHASIBU MKUU WA SHULE YA MSINGI MAKALALA, FEDHA HIZI HAZITORUDISHWA NA KILA MAOMBI YA JENGO YANAJITEGEMEA.

**SHEMU MHENI  
MKUU WA SHULE  
SHULE YA MSINGI MAKALALA**